

MATUMAINI PROG NO:2521

TITLE: UNSHAKABLE SECURITY

SUMMERY: KINAZUNGUMZIA KUHUSU USALAMA USIOTIKISIKA KATIKA KRISTO.

TEXT: WAEBRANIA 12:25-29.

MADA: USALAMA USIOTIKISIKA.

.....

Natuombe;

OMBI.... Jehovah Nissi, Jehovah Shammah, Jehovah Rafa; tunakushukuru kwa ulinzi na uwepo wako. Tunapolianza somo hili la leo kuhusu Usalama ulio Imara, fungua mioyo yetu ili tulielewe vyema. Katika jina la Yesu, Amina.

Rafiki yangu, ni wakati mwingine wa kufurahi kwa kuwa Mungu wetu ametujalia tena nafasi ya kujifunza kutoka katika Neno lake. Ni tumaini langu kwamba unaendelea vyema. Karibu tuanze somo letu la leo lenye kichwa kisemacho.....*Usalama Usiotikisika.*

Kumbuka tu ya kwamba malengo yangu ya kupatana nawe kuptia kwenye idhaa hii ,, bila shaka ni kufundishana kulihusu neno lake Mwenyezi Mungu.

**Hiki ni kipindi cha Matumaini kutoka TWR Kenya.
Mada ya ya leo ni,,, *Usalama Usiotikisika.***

Somo ni kutoka kwenye Waebrania 12:25-29.

Tutakapo kuwa tukihitimisha fundisho leo,, nitakuwa na kupatia anwani ya mawasiliano kati yangu nawe.

Nataka kwanza kabisa ukabarikiwe kupitia kwa wimbo huu

WIMBO:

Ni kweli kabisa ya kwamba Fadhili zake Kristo hazibadiliki kamwe na yeye atabakia kuwa Mwema kila wakati .Asante sana mtumishi Janet Jimmy kwa wimbo huo kwa jina Mwamba.....

Mimi naitwa, Vincent Amara.

Mpendwa,,kila Mkristo humu ulimwenguni,,,kipindi cha Pasaka huwa ni sherehe kubwa tena zaidi. Siku hiyo huwa ni wakati wa kusherehekea ushindi wa Yesu Kristo juu ya mauti kupitia ufufuo wake. Ufufuo huo ni msingi wa tumaini letu na uthibitisho kwamba Mungu ana mamlaka juu ya maisha na hata juu ya kifo.

Lakini katika ulimwengu wa sasa, watu wengi sana wanaishi katika hali ya kutokuwa na uhakika.

Rafiki yangu ,, ya Kesho hayajulikani maana Mambo hubadilika kwa haraka tena zaidi.

Mataifa hubadilika, uchumi hubadilika, afya hubadilika, na hata maisha ya mwanadamu yanaweza kubadilika kighafla.

Swala la Kutokuwa na uhakika ndugu yangu,,, huleta hofu, wasiwasi, na hata kukosa amani.

Hapa kunalo swali muhimu tena zaidi ya kwamba; Je, kuna usalama wa kweli katika ulimwengu unaobadilika kila siku?

Tukizama kwenye neno takatifu,,,bila shaka tunaenda kulipata jibu ambalo ni la wazi tena zaidi.

Ndiyo, kuna usalama usiokuwa wa kutikisika,,,usalama huo unapatikana katika Mwenyezi Mungu.

Sasa tukiingia kwenye neno katika waraka huu kwa Waebrania 12:25-29 ,,Bibilia inasema hivi;

25. Angalieni msimkatalie yeye asemaye. Kwa maana ikiwa hawakuokoka wale waliomkataa yeye aliyesema duniani, zaidi sana sisi hatutaokoka sisi tukijiepusha na yeye asemaye kutoka mbinguni;

26. sauti yake wakati ule iliitikisa nchi;

27. Na neno hili, Mara moja tena, laonyesha kuondoshwa kwa vitu vinavyotikisika, kama vile vilivyofanywa, ili visivyoweza kutikiswa vibaki.

28. Basi tukipokea ufalme usioweza kutetemeshwa, na tuwe na neema, ambayo kwa hiyo tumtumikie Mungu kwa kumpendeza, pamoja na unyenyekevu na kicho.

29. Maana Mungu wetu ni moto ulao.

Ndugu pamoja na dadangu,,kutokana na aya hizi ambazo tumezishiriki kwa pamoja,,tunaweza kuyapata maneno kadhaa ya kusisimua ambayo yanapaswa kutupeleka kwenye usalama usiotikisika.

Kwanza kabisa,,,katika aya ya 25 tunaweza kuyapata maneno mawili,,,maneno hayo ni haya,,,Mengi Zaidi.

Ningependa ukaweze kuuona uhusiano kati ya maneno haya,,,,,yaani Mtu ambaye alizungumza duniani hangeweza kukataliwa.

Ninapendekeza kwamba mmoja alikuwa Musa. Musa alipozungumza kutoka Mlima Sinai na kutangaza mapenzi ya Mungu kama alivyosikia, kila amri ambayo alinena ilikuwa ya uhakika. Hawakuweza kukataliwa. Mungu alizungumza na watu hao yaani Wana-Waisraeli kupitia kwa Musa.

Tunapolirejelea neno kwenye kitabu cha Kutoka 19:16-19,,,tunapata kuyaona maelezo ya kina.

Kwenye Kifungu hiki,,, tunajifunza mambo muhimu yanayotupa usalama wa kweli. Mungu Amezungumza na zaidi Sana tunapaswa Kumsikiliza rafiki yangu.

Katika Waraka huu kwa Waebrania,,tunakumbushwa jinsi ambavyo Mungu alivyozungumza zamani kupitia kwa mtumishi wake Musa katika Mlima Sinai.

Neno linatuambia kwamba,,,Kulikuwa na mungurumo,umeme,moto,sauti ya tarumbeta, na hata mlima huo uliotikiswa kwa nguvu kuu tena zaidi.

Tunafahamishwa ya kuwa,,,,,watu waliogopa sana kiasi kwamba hawakuweza kuistahimili sauti ya Mungu.

Lakini katika aya ya 25 kwenye Waraka huu kwa Waebrania 12:25-29 ,,Biblia inatuhimiza hivi,,, “Zaidi sana sisi hatutaokoka sisi tukijiepusha na yeye asemaye kutoka mbinguni.”

Msikilizaji wangu,,,hiyo ina maana ya kwamba,,,, kama watu hawakuweza kuipuuza sauti ya Mungu zamani, basi sisi leo tunapaswa kuwa waangalifu zaidi kuisikiliza sauti ya Mungu kupitia kwa Bwana wetu Yesu Kristo na Neno lake.Mungu wetu anazungumza nasi kupitia kwa Mwanawe Yesu Kristo.

Kwa maelezo na ufafanuzi zaidi,,haya tunayapata kwenye Waraka huu kwa Waebrania 1:1-2.

Usalama wako wa kweli pamoja na wangu rafiki,, bila shaka huanzia pale,,,tu,,,,tunapolisikiliza Neno la Mungu na zaidi sana kulitii.

Dunia inaweza kubadilika, lakini Neno la Mungu halibadiliki kamwe.

Pili ni kwamba,,,Mungu Atatikisa Vitu Vyote Vinavyotikiswa.

Kwenye aya za 26-27,,kwa mhtasarari neno linasema; “Mara moja tena sitatikisa si dunia tu, bali na mbingu pia.”

Hii inaonyesha kwamba siku moja Mungu atatikisa kila kitu kinachotegemewa na mwanadamu,,,yaani,,,falme za dunia,utajiri, mifumo ya kibinadamu,na zaidi sana nguvu za dunia hii.

Ndugu pamoja na dadangu,,,historia inaonyesha kwamba falme nyingi zimeinuka na kuanguka. Mataifa yenye nguvu yalidumu kwa muda kisha yakapotea. Lakini Mungu anasema kwamba,,,kutakuwa na vitu vitakavyosalia baada ya mtikisiko huo.

Swali kuu ni kwamba,,,vitu hivi ni vigani?

Vitu hivi ni vile vilivyo vya milele na zaidi mno vilivyojengwa juu ya Mungu.

Mpendwa,,,vitu vyote vya ulimwengu huu vinaweza kutikitisika,,,, lakini kile kilichojengwa katika Bwana wetu Yesu Kristo kitasalia kuwa imara.

Na hii ndiyo maana Mkristo awaye yote,,,hapaswi kuweka tumaini lake katika vitu ambavyo ni vya muda tu kama vile,,,fedha,mali,vyeo,au hata nguvu za kidunia.

Mkristo mwenzangu,,,tumaini letu linapaswa kuwa katika Mungu ambaye habadiliki kamwe.

Jambo jingine ni kwamba,,,Ufalme wa Mungu Hauwezi Kutikiswa

Bibilia katika aya ya 28 kwenye Waraka huu kwa Waebrania sura hii ya 12,,,inasema; Basi tukipokea ufalme usioweza kutetemeshwa, na tuwe na neema, ambayo kwa hiyo tumtumikie Mungu kwa kumpendeza, pamoja na unyenyekevu na kicho.

Na hii bila shaka ndiyo habari njema kuu kwa kila muumini.

Falme za dunia zina mwisho, lakini ufalme wa Mungu ni wa milele.

Hakuna nguvu inayoweza kuuangusha,,,hakuna adui anayeweza kuushinda na zaidi sana hakuna mtikisiko unaoweza kuuharibu.

Tunapokuwa sehemu ya ufalme wa Mungu, tunapata usalama wa kweli wa kiroho.

Na ndiyo maana katika Injili ya Yohana 14:1,,,neni linatumbia ya kwamba Yesu kwa wakati mmoja aliwaambia wanafunzi wake maneno haya ya kuwafariji kabla kusulubiwa kwake ya kwamba; “Msifadhaike mioyoni mwenu; mmwamini Mungu, niaminini na mimi.”

Mpendwa,,,usalama wa kweli haupatikani katika mazingira mazuri ya maisha,,,bali unapatikana katika kuwa karibu na Mungu.

Mwisho ni kwamba,,,tunahitaji Neema ya Mungu.

Kwenye aya ya 28 Biblia inasema;Basi tukipokea ufalme usioweza kutetemeshwa, "na tuwe na neema", ambayo kwa hiyo tumtumikie Mungu kwa kumpendeza, pamoja na unyenyekevu na kicho.

Kunayo maneno haya maanne kwamba,,“Na tuwe na neema.”

Neema ni zawadi kutoka kwa Mungu maana sisi wenyewe hatuwezi kuizalisha.

Ni neema ya Mungu tu,,,ndiyo inayotuwezesha,,kusimama imara,inayotuwezesha kumtumikia Mungu, inayotuwezesha kuyashinda majaribu,na zaidi ya yote ndiyo inayotusaidia kuendelea katika imani.

Bila ya kuwepo kwa neema yake Mwenyezi Mungu, sisi ni viumbe dhaifu tu. Lakini neema ya Mungu hutupa nguvu za kuyaishi maisha ya kumpendeza yeye.

Msikilizaji wangu,,,sisi kama viumbe vyake,,tunapaswa kumkaribia Maulana kwa,,heshima,unyenyekavu, na zaidi mno kwa kicho chake,,,maana Biblia inatuambia kuwa; “Mungu wetu ni moto ulao.”

Hiyo inaonyesha utakatifu na ukuu wake mkuu.

Kwa kumalizia mpendwa,,,nataka kukuambia hivi,,,dunia hii imejaa kutokuwa na uhakika. Lakini ndani ya Bwana wetu Yesu Kristo kuna usalama usiotikisika.

Tunapoisikiliza sauti yake Mwenyezi Mungu,tunapolishikilia Neno lake, tunapoingia katika ufalme wake,bila shaka tunapata msingi ambao hautatikiswa kamwe.

Mambo mengi duniani yatapita,,,yaani mataifa,mali ya ulimwengu huu,nguvu,na hata mifumo ya wanadamu.

Lakini ufalme wa Mungu utadumu milele.

Usiweke tumaini lako katika vitu vinavyopita,,,bali liweke tumaini lako katika Mungu aliye hai,,,maana ndani yake mna amani,tumaini na zaidi sana usalama wa milele.

Ningependa kukuacha na kifungu hiki cha kukutia moyo kutoka kwenye Zaburi 46:1-2 ,,,ambacho kinasema hivi; “Mungu kwetu sisi ni kimbilio na nguvu, Msaada utakaoonekana tele wakati wa mateso. Kwa hiyo hatutaogopa.”

Natumai ya kwamba umepata kitu kizuri kutokana na fundisho hili la leo;

Ombi.....

Uliye tukuka Juu ya vyote na tena Mfalme wa wafalme,,tunakushukuru kwa ajili ya fundisho hili leo kuhusiana na usalama usiotikisika. Kwa kweli tutalizingatia kupitia kwa usaidizi wa Roho wako Mtakatifu.

Ni kwa Yesu tumeomba.....Amen.....

Rafiki yangu,,hiki Kimekuwa ni kipindi chako cha kujifunza neno Lake Mwenyezi Mungu. Kipindi cha matumaini kutoka Twr.Leo mada yetu imekuwa ni;Usalama usiotikisika.

Tumeutoa kwenye Waraka kwa Waebrania 12:25-29.

Nitakuomba uwasiliane nami kupitia kwa anwani nitakayo kusomea mwishoni mwa kipindiki hiki cha leo. Anwani hiyo ni kwa ajili ya kusaidiana nawe.

Kabla yake,,u hapa wimbo,, Kwa Yesu kuna usalama.....

WIMBO.....

Na kwa kweli kabisa Kwa Yesu kunao usalama akiwa mtumishi Edson Lufunguro na wimbo kwa Yesu Kuna usalama....Asante sana Bro Edson kwa wimbo huyo wa kutia Moyo.

ANDIKA BARUA AU UJUMBE WAKO UKIANZA NA NENO MATUMAINI TWR NA

KUTUMA KWA:

SLP 21514 CODE 00505

NAIROBI KENYA x2

Simu/Sms 0721970520 x2

Barua Pepe-barua@twr.co.ke

Kwenye Youtube ni @twr.co.ke

Mungu na akubarki sana Msikilizaji popote ulipo na,, hadi wakati mwingine, jina langu ni Vincent Amara.....Kwaheri